# Fantasia Katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto

*Leonard Herman*

*Ikisiri*

Fasihi simulizi na andishi kwa pamoja huchangia sifa moja ya kuwa sanaa ya lugha katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii husika. Hii ndiyo ithibati ya sanaa yoyote kuwa fasihi. Kama uwasilishaji wa mawazo katika jamii utafanyika bila kutumia lugha kisanaa basi hapo hakuna fasihi. Katika kutumia lugha na mbinu nyingine za kisanaa katika kufikisha ujumbe kwa jamii, hasa ya watoto, wakati mwingine kuna kuvuka mipaka ya uhalisia kwa kuhusisha wahusika na mambo ya kinjozinjozi au kifantasia kwa makusudi. Mtindo huu wa kutumia fantasia katika kazi za fasihi ni kinyume kabisa na wanataaluma wanaoamini katika ukweli na uhalisia. Wafuasi wa nadharia ya uhalisia wanadai kuwa mwandishi au msanii wa kazi za fasihi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku (Wafula na Njogu, 2007). Swali la kujiuliza hapa ni kuwa, kwa kuwa fantasia inaukimbia ukweli wa uhalisia katika kazi za fasihi hasa kwa watoto, je, mbinu hiyo ina dhima gani kifasihi? Makala haya yana lengo la kushughulikia swali hilo.

## 1.0 Utangulizi

Fantasia ni hali ya uajabuajabu au undotondoto unaojitokeza katika kazi za fasihi. Kazi ya fasihi ya Kiswahili yenye fantasia ni ile ambayo imesheheni mambo ya ajabuajabu, ya kinjozi, majitu ya kutisha, nguvu zisizo za kawaida, na kadhalika. Mambo haya hayatarajiwi kutokea na hutokea nje ya kanuni na sheria za fasihi katika jamii zetu na ulimwenguni pia. Lakini pia mambo hayo yasiyo ya kawaida hutumika pamoja na uhalisia. Fantasia nyingi huwa na motifu za safari, au msako wa utafutaji au ufumbuzi wa kitu fulani. Mambo ya kifantasia sio ya kweli yaani hayawezi kutokea na hayatarajiwi kutokea isipokuwa hutumiwa kwa makusudi ili kukidhi haja fulani za kifasihi.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa fantasia ni sawa na njozinjozi. Ni dhana inayotumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka uhalisi. Anaendelea kufafanua kuwa ni kazi yenye sifa za kindotondoto au za kutaka kuaminisha hali isiyo ya kawaida. Fantasia hutumika zaidi katika maandishi yanayolenga hadhira ya watoto. Hutumiwa katika kazi za kinathari ambazo huwa na mandhari ya ajabu, matukio magumu kukubalika katika hali ya kawaida na hata wahusika wasioweza kupatikana katika uhalisia. Kutokana na fasili hiyo ya Wamitila, tunaweza kusema kuwa wahusika katika kazi zenye fantasia ni kama vile mazimwi, mashetani, majini na vitu vingine ambavyo havidhaniwi kuwapo katika jamii, yaani haviwezi kupatikana katika uhalisia.

Matumizi ya fantasia katika fasihi ya watoto ni suala la kawaida kwa kuwa ni sifa mojawapo ya kundi hilo la fasihi. Matumizi ya fantasia yanapojitokeza

katika fasihi ya watu wazima huleta upya fulani ambao unakuwa haujazoeleka na hivyo kuwashtua wahakiki wa fasihi. Mshtuko huu ndio uliozaa istilahi ya *uhalisiamazingaombwe* kama inavyotumiwa zaidi na Senkoro (2006: 37). Dhana hii ya uhalisiamazingaombwe inatumika kuzieleza zile kazi za kifasihi zinazounganisha uhalisi na uajabuajabu. Senkoro anaendelea kufafanua kuwa katika kazi za fasihi ya watu wazima,[1] upya huu unaonekana katika riwaya fupi za Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile*, na pia katika kazi mbalimbali za Said Ahmed Mohamed kama vile riwaya yake ya *Babu Alipofufuka* na hadithi fupi ya *Sadiki Ukipenda*, pia katika kazi za Shaaban Robert kama vile *Kusadikika, Kufikirika* na *Adili na Nduguze*. Kama ilivyoelezwa hapo awali, matumizi ya fantasia katika kazi za fasihi ya Kiswahili ya watu wazima kwa kiasi fulani huleta upya. Upya huo unatokana na mazoea kuwa fantasia imezoeleka zaidi kutumika katika fasihi simulizi hasa ndani ya ngano, visasili, visajanja, visapanda, vitendawili na tanzu nyingine za fasihi hii ambazo zimekuwapo karne nyingi.

Makala haya yanaangazia dhima ya matumizi ya fantansia katika fasihi ya Kiswahili kwa watoto. Hili linatokana na ujitokezaji wa mara kwa mara wa sifa hii katika kazi nyingi za watoto hali ambayo inakiuka uhalisia unaoamini kuwa fasihi ni kioo cha jamii. Fasihi kama kioo cha jamii inapaswa kuakisi kile kinachotokea bila kukipotosha kwa kuingiza mambo yasiyo halisi. Kwa kuwa mbinu hii ya kifani hujitokeza katika kazi nyingi za watoto, makala yatatumia kazi mbili tu kama sampuli: hadithi ya *Marimba ya Majaliwa* iliyoandikwa na Edwin Semzaba (2008) na hadithi ya *Bahati na Mumewe* kitabu kilichoandikwa na Debora Mwenda (1995). Kazi hizi zimeteuliwa kwa kigezo cha uwakilishi sawa wa kijinsia, yaani moja imeandikwa na mwanaume na nyingine imeandikwa na mwanamke. Kwa kuwa makala yatamakinikia fasihi inayolenga hadhira ya watoto, pengine ni bora tukazungumzia walau kwa ufupi juu ya fasihi ya watoto.

## 2.0 Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto[2] ikilinganishwa na ile ya watu wazima si fasihi kongwe. Historia na maendeleo yake duniani inahusianishwa na kutambuliwa kwa hatua ya utoto na nafasi ya mtoto katika jamii. Fasihi ya watoto daima iliathiriwa na mtazamo waliokuwa nao wakubwa juu ya watoto. Kwa hali hiyo, kama ikichukulia kuwa fasihi ya watoto inawahusu watoto kama hadhira na siyo kile kinachowasilishwa na mwandishi, itakubalika kuwa fasihi ya watoto haikuwapo

[1] Fasihi ya watu wazima ni ile yenye dhamira zinazolenga hadhira yenye umri wa miaka 18 na zaidi.
[2] Makala haya yatachukulia kuwa mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya miaka 18, aliye chini ya uangalizi wa mtu mzima kimalezi yaani, ambaye bado hajapewa uhuru kamili kijamii wa kujitawala kiakili, kimaamuzi, na kadhalika.

hadi ilipofika katikati ya karne ya 18. Wakati huu ndipo mtoto alitambuliwa kama kiumbe wa pekee na kwamba ana umuhimu wake katika familia na kwenye jamii. Tunaweza kusema kuwa hapa ndipo fasihi ya watoto ilipoanza. Kabla ya karne ya 12 kipindi cha utoto kilionekana kama kipindi cha mpito tu badala ya kipindi maalumu cha makuzi. Maelezo hayo yanatoa picha juu ya uchanga wa fasihi ya watoto duniani. Lakini, makala hayana nia ya kuangalia uchanga huo bali mtindo wa fantasia unaopendwa kutumiwa na wasanii wa kumbo hili.

Kuna mitazamo mbalimbali kuihusu fasihi ya watoto. Kwa mfano, Wamitila (2010) anasema kuwa suala la ufafanuzi wa fasihi ya watoto linaweza kueleweka kwa kukitwa katika mitazamo mikuu miwili. Mosi, fasihi ya watoto ni ile ambayo hadhira yake ni watoto. Pili, fasihi ya watoto ni ile ambayo msingi wa kidhamira na kimaudhui huwarejelea watoto. Lakini pia, ieleweke kuwa, nje ya mitazamo hiyo mtazamo mwingine unaweza kuwa fasihi ya watoto ni ile iliyoandikwa au kusimuliwa na watoto wenyewe.

Kwa kujikita katika kigezo cha umri, fasihi ya watoto ni ile inayowahusu watu walio chini ya umri wa miaka 18. Fasihi hiyo inakuwa na sifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa na michoro mingi mizuri na ya kuvutia (kama ni andishi), kuandikwa kwa kutumia lugha rahisi inayoeleweka kwa watoto. Kazi hizo husheheni pia mbinu za kifantasia, na mara nyingi huwa na wahusika watoto (hasa wahusika wakuu). Kazi nyingi hukitwa katika motifu ya safari na msako. Aghalabu kazi hizo zina muundo sahili, siyo ndefu kupindukia, zinajali saikolojia ya watoto, na kadhalika. Fasihi ya watoto inaweza kuwa ni riwaya, hadithi fupi (bunilizi), tamthilia, ushairi, hadithi au semi.

## 3.0 Muhtasari wa Hadithi Teule na Fantasia Inavyojitokeza

### 3.1 Hadithi ya *Marimba ya Majaliwa*

*Marimba ya Majaliwa* ni hadithi iliyoandikwa na Edwin Semzaba na kuchapishwa mwaka (2008). Hadithi hii inaanza na tukio la mashindano ya kumsaka bingwa wa kupiga marimba huko kisiwani Mafia. Tukio hilo linafuatiwa na kuibiwa kwa marimba ya Majaliwa yenye nyuzi ishirini (ukurasa wa 2). Marimba hii ilikuwa ya ajabu sana kwani ikipigwa watu wote katika mashindano walikuwa wanashangilia kwa furaha. Marimba hiyo aliyoipenda sana Majaliwa iliporwa na Kongoti Nachienga aliyekuwa bingwa wa kitaifa katika kupiga marimba. Kongoti Nachienga aliiba marimba hiyo kwa msaada wa babu mzaa baba wa Majaliwa. Marehemu bibi mzaa mama yake Majaliwa aliamua kuingilia kati ili kuhakikisha mjukuu wake anapata marimba hiyo.

Hadithi hii inaendelea kuelezea msako wa marimba hiyo katika mikoa mbalimbali ya Tanzania. Msako huo unaanzia katika Kisiwa cha Mafia katika shindano la kumsaka mpiga marimba mahiri ambaye angewakilisha mkoa wa Pwani katika mashindano ya kitaifa huko Dodoma. Safari ya kusaka marimba haikuwa rahisi kwa Majaliwa kwani ilijaa vituko vingi vya kishirikina kati ya marehemu babu na bibi yake Majaliwa. Majaliwa alipitia masaibu ya hapa na pale. Lakini kwa kuwa bibi yake alikuwapo kifantasia mambo yote yaliwezekana mpaka ushindi ukapatikana. Kwa kiasi kikubwa Majaliwa alifanikiwa kupambana na hali ngumu katika safari hiyo kwa msaada wa jiwe la rubi alilopewa na marehemu bibi yake. Jiwe hilo lilikuwa na uwezo wa kufuata masharti ya Majaliwa. Kwa mfano, jiwe hilo aliweza kuliagiza kuhamisha chakula au vinywaji kutoka tumboni kwa mtu mwingine mpaka tumboni kwa Majaliwa na lilifanya hivyo.

Misukosuko mingi aliyokumbana nayo Majaliwa ilitokana na vita au mvutano mkubwa uliokuwapo kati ya marehemu babu mzaa baba na bibi mzaa mama yake ambao walikuwa mahasimu enzi za uhai wao. Mizimu hiyo ilikuwa na mivutano mikubwa sana ndiyo maana iliamua kuanzisha ugomvi kupitia Kongoti Nachienga na Majaliwa. Bibi alimsaidia Majaliwa na Kongoti Nachienga alisaidiwa na babu mzaa baba yake Majaliwa. Kwa kuwa mizimu hiyo ilikuwa na uwezo mkubwa kupita ule wa binadamu aliye hai, vita hivyo vilikuwa vikali sana lakini hatimaye Majaliwa alifanikiwa kushinda kwa kuipata marimba yake iliyokuwa inampatia ushindi daima. Hadithi inashia kwenye mashindano huko Dodoma ambapo Majaliwa baada ya kupata marimba yake aliipiga na kushika namba moja katika mashindano.

### 3.2 Fantasia inavyojitokeza katika Hadithi ya *Marimba ya Majaliwa*

Katika hadithi hii kuna mambo kadhaa yanayotumiwa na mwandishi ambayo katika ulimwengu halisi hayawezi kutokea. Kwa mfano, tutazame dondoo zifuatayo:

Kwanza, uwezo wa ufagio na ungo kuruka angani. Katika simulizi hii tunaambiwa na mwandishi kuwa bibi na Majaliwa walisafiri sana kwenda sehemu nyingi nchini Tanzania kwa kutumia ufagio (ukurasa wa 22) na ungo (ukurasa wa 80).

Pili, uwezo wa bibi na babu yake Majaliwa wa kujigeuza kuwa katika umbo lolote wanalotaka. Kwa mfano, katika ukurasa wa 6 bibi alijigeuza kuwa papa na mara taratibu akaanza kujibadilisha na kuwa nguva na nusu mtu. Ukurasa wa 143 mwandishi ameonesha jinsi bibi alivyogeuka na kuwa tai. Katika ukurasa wa 5-7 bibi anajitokeza katika umbo la samaki na kumbeba Majaliwa.

Tatu, uwezo wa jiwe la rubi. Katika sehemu nyingi ndani ya hadithi hii, Majaliwa anaonekana akiokolewa katika mikasa mingi na jiwe lake la rubi. Jiwe hili ni la ajabu kwani liliweza kutii amri za majaliwa kama vile kuhamisha chakula au kinywaji kutoka kwa mtu mwingine hadi tumboni mwa Majaliwa, kumzamisha mamba, na kadhalika.

Nne, uwezo wa mamba kutumwa na binadamu kufanya uhalifu. Babu yake Majaliwa alimtuma mamba amshambulie Majaliwa lakini kwa bahati nzuri Majaliwa akawahi kushika rubi yake na kufanikiwa kujiokoa. Hali hii si ya kawaida katika ulimwengu halisi (ukurasa wa 46).

Tano, uwezo wa upepo kuwa ndege mkubwa. Katika ukurasa wa 169 na 170 msimulizi anatuambia kuwa mvuvi mmoja alikuwa katika shughuli zake za kuvua na akavua chupa, alipoifungua ikapasuka na kumwangusha mvuvi. Taratibu ule upepo mkali ulianza kubadilika na kuwa ndege mkubwa sana.

Sita, jiwe kuzunguka lenyewe bila kuguswa na mtu. Majaliwa alipofika Ukerewe aliona mawe mawili makubwa juu ya mlima ambapo jiwe moja la juu lilikuwa linazungukazunguka. Hali hii katika mazingira ya kawaida si halisi na wala hatutegemei kuona jiwe likizunguka lenyewe bila mtu kuligusa.

Saba, kuwepo kwa viumbe waitwao vibwengo wanaotumwa kumshambulia mtu. Wakati Majaliwa akiwa angani na bibi yake babu yake alituma vibwengo ili viwashambulie lakini bibi alikabiliana navyo (ukurasa wa 53). Majaliwa aliona kundi kubwa la vibwengo likiwajia kutoka kushoto, kulia na mbele yao. Pia, kurasa za 27, 58, 93 na 194 mwandishi anaonesha jinsi babu yake Majaliwa alivyotuma vibwengo kumkabili bibi na Majaliwa. Hawa viumbe hawana uhalisia bali ni wa kudhaniwa tu akilini.

Nane, kusafiri kwa njia ya kufumba na kufumbua. Bibi alikuwa akimwambia Majaliwa afumbe macho na akifumbua wanakuwa wamefika sehemu au eneo lingine. Mfano, ukurasa wa 107, bibi alimwambia Majaliwa afumbe macho baada ya kufumbua macho alijikuta yumo ndani ya pango la Amboni.

Hiyo ni baadhi tu ya mifano michache ya namna fantasia ilivyojitokeza katika hadithi ya *Marimba ya Majaliwa*. Yapo mambo mengi sana katika hadithi hii yanayofanana na hayo yaliyotolewa kama mifano. Mambo hayo yanaweza kutokea katika ulimwengu wa kufikirika tu, kiuhalisia hayapo na wala hayawezi kuthibitishwa kisayansi.

**3.3 Hadithi ya *Bahati na Mumewe***

Hadithi hii inatoka katika kitabu cha Debora Mwenda *Bahati na Mumewe* (1995). Hadithi inamhusu Bahati ambaye alikuwa binti pekee wa Bwana Jojo na mkewe. Binti huyu alikuwa mrembo aliyelelewa katika misingi ya maadili mazuri. Kwa sababu ya uzuri wake na kuwa na tabia nzuri, vijana wengi wa kijiji chao walikuja nyumbani kwao ili kuleta maombi yao ya uchumba. Mara nyingi, Bahati alionywa sana na wazazi wake kuhusu kuolewa na mtu asiyemfahamu. Lakini, mara zote Bahati alipenda kuolewa na mtu wa mbali. Baada ya muda fulani alijitokeza kijana mmoja mtanashati mwenye upendo kwa kila mtu hasa wale wenye shida na pia aliwapenda sana watoto. Kwa sababu ya sifa hizo wanakijiji walimpenda na hivyo kijana huyo alipokwenda kumchumbia, Bahati alikubali kwa urahisi.

Baada ya muda mfupi Bahati akawathibitishia wazazi wake kuwa hata kama hamfahamu kijana yule bado ameamua kwa moyo wake kumpenda. Ndoa ilifungwa na mara safari ya kuelekea kwa muoaji ikaandaliwa. Kabla ya safari binamu yake Bahati aliyeitwa Sina-Kitu aliomba aambatane na Bahati ili apaone sehemu ambapo ndugu yake anakwenda kuolewa. Kwa shida sana Bahati na muwewe Tetemeko walimkubalia Sina-Kitu afuatane nao. Safari ilichukua muda wa siku sita wakitumia usafiri wa farasi. Farasi huyo alikimbia sana na alikuwa na uwezo wa kupita juu ya bahari bila kuzama.

Baada ya kufika kwa Tetemeko maisha yalianza vizuri japo kadiri muda ulivyozidi kwenda shemeji yake Sina-Kitu alizidi kushikwa na wasiwasi kuwa inawezekana binamu yake alikuwa ameolewa na zimwi. Hali hiyo ilimfanya Sina-Kitu aanze utafiti na mwisho akajiridhisha kuwa shemeji yake alikuwa zimwi. Mkakati wa Tetemeko na mazimwi mengine ulikuwa ni kuwanenepesha Bahati na Sina-Kitu ili baadaye waweze kuliwa. Hali hiyo ilimfanya Sina-Kitu kuanza mkakati wa kusuka mkeka utakaowaokoa wakati wa hatari. Muda wa kuliwa ulipofika mazimwi yalianza safari ya kuja nyumbani ili kutimiza azma hiyo. Kwa bahati nzuri Sina-Kitu alikuwa amekwishajiandaa na kuanza kuamuru mkeka kuruka juu. Pamoja na ugumu wa Bahati kuelewa mipango ya mazimwi hatimaye Sina-Kitu alifanikiwa kujiokoa na kumuokoa binadamu yake. Safari ya kurudi kwao kwa kutumia mkeka ilikuwa nzuri na mwisho walifika na kusimulia yote yaliyowapata. Sina-Kitu alipongezwa sana na wazazi wa Bahati kwa juhudi zake za kuhakikisha wanajiokoa.

**3.4 Fantasia inavyojitokeza katika Hadithi ya *Bahati na Mumewe***

Katika hadithi ya Bahati na Mumewe yapo mambo ambayo katika hali ya kawaida hayawezi kudhihirika. Mambo hayo hudhihirika kifikra tu katika masimulizi. Mifano ifuatayo inaonesha fantasia ilivyojitokeza katika hadithi hii.

Mosi, uwezo wa farasi aliyewabeba Tetemeko, Bahati na Sina-Kitu kutembea juu ya bahari bila kuzama. Farasi alikuwa na uwezo wa kuvuka bahari akiwa amewabeba. Katika hali ya kawaida hii haiwezekani.

Pili, uwezo wa Tetemeko na ndugu zake kugeuka kiumbo na kuwa wanyama au majitu ya ajabu. Katika hali ya kawaida kujibadilisha kiumbo haiwezekani. Mwandishi anasema,

> "Hapo Sina-Kitu alitoka nje ya jumba lile kwa haraka, akaenda kupanda katika mti mmoja mrefu. Kwa mbali akaona Tetemeko na ndugu zake huko porini wakianza kuvua nguo zao. Mara mmoja baada ya mwingine akawa anageuka kuwa mnyama wa kutisha mwenye miguu mitano, manyoya mwili wote, makucha marefu na mkia mrefu." (ukurasa wa 21).

Tatu, uwezo wa mkeka kubeba watu na kuruka angani. Mwandishi anasimulia kuwa Sina-Kitu akachukua mkeka na kifurushi chake. Akautandaza mkeka chini, kisha akaamuru,

> Ruka mkeka ruka
> Hadi mawinguni kukuta
> Ruka mkeka ruka
> Kurudi nyumbani kwetu
> Ruka mkeka ruka
> Sina-Kitu nilikotoka
> Ruka mkeka ruka
> Kwa wazazi watukuka.

Mara mkeka ulianza kuruka. Bahati aliyekuwa anachungulia dirishani alishangaa kuona mkeka polepole unapaa angani, huku Sina-Kitu akiwa juu yake (ukurasa wa 30). Mambo haya hayawezi kutokea katika hali halisi wala kudhihirika kisayansi kwa sababu ni ya kindotondoto tu.

## 4.0 Dhima ya Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto

Baada ya kuangalia muhtasari wa vitabu teule na jinsi fantasia inavyojitokeza, bado swali letu halijajibiwa. Kwa kuwa mambo hayo ya kindotondoto si halisi, je, yaepukwe katika fasihi ya Kiswahili kwa watoto? Katika kujibu swali hilo lazima tujiulize swali jingine kuwa, kwa nini waandishi (hasa wa hadithi teule) waliamua kutumia fantasia katika utunzi wao? Nia yao au mchango wa mbinu hiyo kifasihi ni ipi? Sehemu inayofuata itaeleza kwa kina, kwa nini mtindo wa kifantasia umekuwa ukitumika. Sababu kuu za fantasia katika fasihi ya watoto makala haya yanazibainisha kuwa ni pamoja na:

### 4.1 Kujenga Msuko wa Matukio ya Hadithi

Mohamed (1995) anauita msuko huu kuwa ni ploti. Anaifafanua ploti kuwa ni msukumo wa hadithi katika mpangilio fulani. Anazidi kufafanua kuwa msukumo huu hujengwa na wahusika wanaotenda na kutendana na kuathiriana kusababisha matukio, mwendo na kasi ya kwenda kiwakati na pahala. Maelezo hayo ya Mohamed hayatofautiani sana na yale aliyoyatoa Madumulla (2009) kuwa ploti ni usimuliaji wa matukio unaoweka uzito katika usababishaji wa matukio. Akimnukuu Cuddon, Madumulla anasema kuwa ploti huchochea udadisi na taharuki kutokana na kuibua swali la `kwa nini?' Ufafanuzi huo unachukuana moja kwa moja na ule wa Wamitila (2011) unaodai kuwa msuko ni mpangilio wa matukio katika kazi ya kifasihi.

Dhima mojawapo ya kutumia mambo ya kifantasia katika kazi za kifasihi, hasa zile za watoto ni kuibua matukio ili kufanikisha msuko wa hadithi. Katika *Marimba ya Majaliwa* kwa mfano, kuwapo kwa marehemu bibi na babu yake Majaliwa ni kusaidia kusukuma mbele na kufanikisha usimulizi. Mwandishi anaonesha jinsi babu na bibi yake majaliwa walivyokuwa na uhasama wakati wa uhai wao na hatimaye baada ya kufa hali hii ikaendelea huko kuzimuni. Hali hiyo ya uhasama ndiyo inayoweza kujibu swali la kwa nini Kongoti Nachienga aliiba marimba ya Majaliwa. Mizimu hii iliwezesha simulizi nzima kunoga na kuzua taharuki nyingi katika sura mbalimbali. Aidha, katika hadithi ya *Marimba ya majaliwa* matukio yake yote yanayohusu safari za Majaliwa na bibi yake nchi nzima kwa kiasi kikubwa yamefanikishwa kwa fantasia ya matumizi ya kufumba na kufumbua, pia matumizi ya ungo na ufagio kama usafiri kutoka sehemu moja ya matukio kwenda sehemu nyingine.

Halikadhalika, katika hadithi ya *Bahati na Mumewe* mwandishi anayatumia mazimwi kwa sababu hiyohiyo ya kuzua usababishi unaounda msuko wa matukio. Mhusika Tetemeko ambaye ni zimwi pamoja na mazimwi wenzake wanafanikisha msuko wa hadithi kwa kufanya mambo ya ajabuajabu ikiwa ni pamoja na kujigeuza katika maumbo mbalimbali pamoja na uwezo wao wa kumeza watu. Uwezo wa mkeka kupaa angani unafanikisha mchakato wa uokozi wa Sina-Kitu na Bahati. Yote hayo yametumiwa na watunzi ili kufanikisha msuko wa hadithi wenye mvuto na taharuki.

### 4.2 Kujenga Taharuki kwa Wasomaji/Wasikilizaji

Madumulla (2009) anamuelezea msanii mzuri kuwa ni yule anayepanga kazi yake kiasi kwamba tukio moja linasababisha jingine, na kusababisha kujenga hamu ya msomaji ya kutaka kuendelea kujua kulikoni. Hali hii ndiyo huitwa taharuki. Utumizi wa fantasia katika fasihi hasa ya watoto unasaidia sana katika kukidhi haja hii. Mambo ya ndotondoto au ajabuajabu humfanya mtoto azidi

kupata hamu ya kutaka kujua kipi kinafuata baada ya tukio moja au nini hatima ya mtu au kitu fulani. Kwa mfano, Majaliwa anapopewa jiwe la rubi katika hadithi ya *Marimba ya Majaliwa* kama msaada wake wakati wa shida, humfanya msomaji awe na hamu ya kutaka kujua ni kwa vipi jiwe hilo litamsaidia Majaliwa. Lakini pia jiwe linapopotea msomaji hujiuliza hivi itakuwaje kwa Majaliwa bila jiwe la rubi? Zaidi ya hayo, mwandishi anapotambulisha mgogoro mkubwa kati ya marehemu bibi na babu kuwa uliendelea huko kuzimuni na kuibuka upya kupitia kwa Majaliwa na Kongoti Nachienga unamfanya msomaji atake kujua hatima ya hali hiyo itakuwa nini.

Katika hadithi ya *Bahati na Mumewe* Sina-Kitu anaposhikwa na wasiwasi juu ya umbile la shemeji yake na kuanza uchunguzi, humchochea msomaji kutaka kujua matokeo ya utafiti huo. Lakini pia msomaji hujiuliza kuwa kwa vile mwandishi alidokeza kuwa zimwi lile liligundua mikakati yote ya Sina-Kitu ni kipi kingefuata ili kuzima harakati za kusaka ukweli. Hayo yote humtia hamasa msomaji kupenda simulizi na kutaka kusonga mbele zaidi. Ufundi huu Senkoro (2006) anaushabikia kwa kusema kuwa ufundi wa kushikilia hadhira kwa taharuki unaweza kuletwa si kwa yale yanayoelezwa tu, bali pia jinsi yanavyotolewa na msanii/mtambaji. Kwa hiyo, kuchanganya matukio halisi na yale ya kinjozinjozi ni ufundi au mbinu mojawapo inayotumiwa sana na waandishi wa kazi za watoto kwa nia ya kuiteka hadhira kitaharuki.

### 4.3 Kuibua Migogoro ya Hadithi

Msuko wowote ule hauwezi kusogeza mbele hadithi bila kuwa na mgogoro au migogoro baina ya wahusika. Migororo lazima iibuliwe na ufundi wa msanii kwa kuonesha uhasama wa kisanii kati ya mtu na mtu au mtu na jamii yake. Hii hufanya simulizi kusonga mbele na kuwa ya kuvutia sana. Katika hadithi ya *Marimba ya Majaliwa*, mgogoro uliokuwapo kati ya Kongoti Nachienga na Majaliwa akichochewa sana na marehemu bibi na babu wa Majaliwa ndio uliosaidia hadithi kuwa ya kuvutia. Mara msomaji anapoanza kuisoma hadithi hii huvutiwa na simulizi kwa kujengewa ari ya kutaka kujua hatima ya mgogoro huu. Madumulla (2009) anasema kuwa ili kuipa uzito kazi ya fasihi, inafaa msanii awe mwangalifu katika kuwianisha pande mbili zinazogongana. Matumizi ya fantasia yanasaidia sana kufanikisha ujenzi wa migogoro ya kihadithi ili kusongesha masimulizi mbele.

Katika hadithi ya *Bahati na Mumewe*, matendo ya ajabuajabu ya Tetemeko yanaibua mgogoro kati yake na Sina-Kitu. Pia hali hiyo ya uajabuajabu iliibua mgogoro kati ya Sina-Kitu na binamu yake (Bahati). Tetemeko alivyoanza kujigeuza kuwa jitu la ajabu hasa wakati wa kulima akiwa na mazimwi wenzake mgogoro uliibuka kati yake na Sina-Kitu. Nafsi ya Sina-Kitu ilianza

kuhangaika ili kutaka kujua ukweli wa umbile la Tetemeko. Baada ya Sina-Kitu kuanza uchunguzi juu ya umbile na matendo ya Tetemeko, hakuweza kuelewana tena na Bahati na Tetemeko mwenyewe. Mgogoro huu uliojengwa kwa ufundi na mwandishi kwa kutumia matendo ya kifantasia unasaidia sana katika kujenga msuko wa simulizi nzima na pia unasaidia katika kuibua taharuki kwa wasomaji wa hadithi.

### 4.4 Kuibua Dhamira katika Hadithi

Matumizi ya fantasia katika kazi nyingi za kifasihi, hasa kwa watoto, hutumiwa kwa lengo la kuibua dhamira. Masuala kadhaa huibuliwa kupitia mambo ya kiajabuajabu yanayojitokeza. Kwa mfano, katika hadithi ya *Marimba ya Majaliwa* kitendo cha bibi yake Majaliwa kutoa jiwe la ajabu *rubi* kwa mjukuu wake kinaweza kuibua dhamira nyingi kama vile kutoa msaada kwa mtu anapokuwa katika matatizo. Lakini pia jiwe hilo la ajabu linaibua suala la kuwatii wakubwa hasa pale wakubwa hao wanapotoa masharti. Majaliwa kwa kukosa utii, wakati mwingine alipatwa na matatizo makubwa sana baada ya jiwe lake kushindwa kufanya kazi kutokana na ukiukaji wa masharti. Pia, bibi yake Majaliwa anawafunza watoto kutembelea mbuga za wanyama na kujua utajiri mwingi wa nchi yao. Haya yamedhihirika kwa kumpeleka Majaliwa katika maeneo mbalimbali ya nchi ya Tanzania mfano, mlima Kilimanjaro, hifadhi za taifa kama Tarangire, mapango ya Amboni, na kadhalika. Suala jingine linalohusiana na dhamira ni umuhimu wa watoto kuifahamu nchi yao kihistoria, kijiografia, kisiasa na kiutamaduni. Mbinu hii ya kutumia fantasia inafanikisha suala la kuifahamu nchi hasa baada ya kuibua matembezi ya mkoa mmoja hadi mwingine kwa njia za kinjozinjozi (kufumba na kufumbua).

Katika hadithi ya *Bahati na Mumewe* mwandishi anafanikiwa pia kutumia fantasia katika kuibua masuala mbalimbali ambayo ni sehemu ya maudhui. Kwa mfano, mhusika Tetemeko, mtu mwenye uwezo wa kujigeuza zimwi au jitu la ajabu anakuwa kama adhabu kwa mhusika Bahati ambaye hakusikia ushauri wa wazazi wake waliomuasa daima kuolewa na mtu anayemfahamu, tena wa kijijini kwao. Matumizi ya fantasia katika fasihi kama nyenzo ya kuibua na kushadidia dhamira yanaungwa mkono na Mohamed (1995) pale anaposema kuwa japo suala la kutumia fantasia linakiuka uhalisia linakuwa na mantiki katika misingi ya yale mwandishi anayotaka kusisitiza.

### 4.5 Kufanikisha Ujenzi wa Mandhari

Wamitila (2011) anafafanua kuwa mandhari ni neno linalotumiwa kuelezea mazingira, eneo, mahali au wakati wa hadithi inayohusika. Anaongeza kuwa kila hadithi husimuliwa kwenye muktadha fulani kimazingira, kimaeneo, kimahali na kiwakati. Mandhari ni nguzo muhimu katika ujenzi wa kazi ya

kifasihi. Fantansia katika kazi za watoto inatumika kuonesha mandhari yasiyowezekana katika hali ya kawaida kwa binadamu. Kutokana na hili mwandishi anafanikiwa kuwasilisha mawazo changamani. Mfano, Majaliwa kuingia katika tumbo la nyangumi na kutembea katika ulimi wake pamoja na kukaa katika moja ya magego ya nyangumi. Anaendelea kusema kuwa mdomo wa nyangumi ulikuwa mkubwa kama sebule, kitu ambacho kwa hali ya kawaida hakiwezi kutokea. Kutokana na hali hii msanii anaonesha ukomavu wake katika kubuni mandhari hayo ambayo yanamfanya mtoto aweze kufikiri zaidi. Kwa hiyo, kutumia fantasia katika kujenga mandhari kunasaidia pia ujenzi wa dhamira na maudhui ya kazi hiyo.

## 4.6 Kuvuta Usikivu wa Hadhira

Mwandishi au msimulizi wa hadithi kwa watoto lazima awe na uwezo mkubwa wa kuchanganya matini. Matini hizo zinapokuwa za kihalisia tu watoto wanachoka haraka na kuona ni za kawaida. Hali hii inamlazimu msanii kuchanganya mambo halisi na yale ya ajabuajabu ili kuvuta usikivu wa hadhira yake. Msanii lazima wakati akisimulia au kuandika abaki kama chanzo cha fasihi lakini pia wakati huohuo aingie katika kundi la hadhira kifikra ili kuonja na kujua ladha ya kazi yake. Pale anapohisi kuwa hadhira imechoka, au kuzoea kazi yake hulazimika kuchanganya matini ili kuleta upya. Upya huo unamsaidia sana msanii kuendelea kuishikilia hadhira yake katika usimulizi wake. Hapa ndipo utumizi wa mambo ya kifantasia huchukua nafasi kubwa hasa kwa kazi zinazowalenga watoto. Uwezo wa kuchanganya uhalisia na mambo ya kifantasia sio wa kawaida. Matumizi ya fantasia katika kazi za watoto kwa kiasi kikubwa huonesha kiwango cha juu cha msanii cha uelewa alionao juu ya hadhira yake. Ili uweze kuiteka hadhira ya watoto lazima ujue na kuimudu vema saikolojia yao. Kwa hali hiyo, mwandishi au msimulizi wa hadithi anayetumia mtindo huu katika kazi zake hudhihirisha umahiri alionao katika kuisana kazi yake. Hata katika upishi, mpishi mzuri yule anayezijua vyema tabia na mapenzi ya walaji wa chakula chake.

## 4.7 Kutimiza Matamanio ya Binadamu

Binadamu ana uwezo wa kufanya mambo mengi sana katika ulimwengu wa kihalisia. Kwa upande mwingine, yapo mambo mengine ambayo binadamu hutamani kuyafanya lakini hana uwezo nayo. Kila jamii ina utamaduni wake. Kuwa na utamaduni pia huambatana na suala la maadili ambalo huunda mikatale fulani kwa watu wake. Watu wa jamii hiyo hulazimika kuitii mikatale hiyo na hivyo kukosa uhuru wa kufanya au kueleza kila kitu kwa uwazi. Kupitia matumizi ya fantasia, hasa katika fasihi ya watoto, mambo yote hata yale yasiyowezekana kwa binadamu huwezekana. Mambo yale yanayobanwa

na mikatale ya kijamii huwezekana kuyasema kupitia kazi za kifasihi kupitia fantasia.

Sigmund Freud katika nadharia yake ya saiko-changanuzi anaifananisha kazi ya fasihi na ndoto. Anaeleza kuwa kwa kuwa kazi za fasihi kama riwaya, tamthilia na ushairi ni kazi za ubunifu, kazi hizi ni sawa tu na ndoto ya mtunzi. Hata wahusika wanaopatikana katika fasihi ni wanadamu wanaoishi katika ndoto na njozi za mwandishi (Wafula na Njogu, 2007). Kwa mawazo hayo ya Sigmund, matumizi ya fantasia katika kazi za fasihi huonesha matamanio ya mtunzi. Mambo ya ajabuajabu au kinjozinjozi yanayotumiwa na waandishi katika kazi za watoto huonesha jinsi ambavyo waandishi hao wanatamani kufanya mambo fulani fulani. Kwa mfano, Kutokana na serikali za nchi nyingi kubuni namna ya kupata fedha za kuendeshea shughuli za maendeleo kwa wananchi na utawala kwa ujumla, wanyama wa msituni wamewekwa chini ya uangalizi maalumu, ili wale wanaotaka kuwaona walipie. Udhibiti huu huwa kikwazo kwa wenyeji wa maeneo hayo. Nchini Tanzania kwa mfano, huwezi ukaingia kwenye mbuga za wanyama, mapango muhimu kama Amboni, na kupanda mlima Kilimanjaro bila kutoa fedha ya kiingilio. Ukiingia bila kibali unaweza kuchukuliwa hatua kali (hii ndiyo mikatale ya jamii). Kwa kutumia fantasia katika fasihi ya watoto, msanii anaweza kuipeleka hadhira yake katika mbuga, mapango adimu au milima muhimu kama Kilimanjaro. Hili ndilo alilolifanya Semzaba kwa kuwatembeza watoto wa fasihi ya Kiswahili mbugani, mapangoni na mlima Kilimanjaro kifikra katika hadithi ya *Marimba ya Majaliwa*.

### 4.8 Kumfikirisha Msomaji/Msikilizaji nje ya Ulimwengu Halisi

Ujenzi na upangaji mzuri wa wahusika, mandhari na vitu vya kinjozinjozi huwafanya watoto watalii katika ulimwengu mwingine ulio nje ya ule wanaoujua. Matumizi ya fantasia kupitia wahusika wanaotisha kama mazimwi, majini na vitu visivyoonekana humfikirisha zaidi mtoto. Mfano, katika kitabu cha *Marimba ya Majaliwa,* mtunzi ameamua kumtumia bibi yake Majaliwa ambaye alifariki siku nyingi. Bibi huyu kwa kuwa alikuwa mzimu alikuwa na uwezo wa kujibadilisha kiumbo na alikuwa anaweza kufanya mambo mengi ambayo binadamu hai hawezi kuyafanya. Kwa hali hiyo waandishi wanatumia fantasia ili kumpa msomaji uwezo wa kufikiri zaidi ya mambo anayoyaona katika ulimwengu halisi. Kumfikirisha mbali msomaji hasa mtoto humsaidia katika kukuza kiwango chake cha kufikiri.

### 5.0 Hitimisho

Kutokana na mjadala na umuhimu wa fantasia katika fasihi ya watoto, makala haya yanahitimisha kwa kusisitiza kwamba kwa vile matumizi ya fantasia yameonekana kuwa sehemu ya ubunifu wa msanii katika kuibua dhamira na

maudhui mbalimbali katika kazi za fasihi, basi mbinu au mtindo huu uendelee kutumika. Pamoja na kuwa fasihi ni kioo cha jamii, si lazima mambo yote yaelezwe kwa kutumia uhalisia. Mambo mengine yanaweza kuakisiwa kwa mbali zaidi hasa kwa kutumia matukio ya kifantasia. Msimamo wa makala haya ni kuwa kujenga kazi ya fasihi kwa kuchanganya uhalisia na fantasia ni ubunifu wa kiwango cha juu katika fasihi ya watoto.

## Marejeo

Kezilahabi, E. (2011). *Mzingile*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Kezilahabi, E. (2011). *Nagona*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mohamed, S.A. (2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S.A. (2007). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mwenda, D. (1995). *Bahati na Muwewe*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.

Njogu, K. na R. M. Wafula. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Robert, S. (1951). *Adili na Nduguze*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Robert, S. (1991). *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robert, S. (2008). *Kufikirika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Semzaba, E. (2008). *Marimba ya Majaliwa*. Dar es Salaam: E&D Publishers Limited.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi (1): Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*.Nairobi: Vide~Muwa Publisher Limited.

Wamitila, K. W. (2011). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.